



HESLB
BODI YA MIKOPO
TUNAWEKEZA KWA KIZAZI CHA BAADAE



MWONGOZO

UTOAJI MIKOPO NA RUZUKU
KWA SHAHADA YA KWANZA

2022/2023

Unapatikana

www.heslb.go.tz

#WeweNdoFuture
TimizaWajibu

HESLB TANZANIA



HESLB_TANZANIA



Maelekezo Muhimu kwa Wanafunzi Wote Waombaji wa Mikopo

Waombaji mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2022/2023 wanafahamishwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- (i) Kusoma na kufuata taratibu za maombi katika Mwongozo huu wa mwaka wa masomo 2022/2023;
- (ii) Kuhakikisha kuwa namba ya mtihani wa kidato cha nne iwe sawa kwenye maombi ya mkopo na udahili wa chuo;
- (iii) Waombaji ambao wamefanya mtihani wa kidato cha nne zaidi ya mara moja wahakikishe wanaorodhesha namba zote katika maombi yao;
- (iv) Kuhakikisha kuwa nyaraka zote za maombi ya mkopo unazowasilisha ziwe zimehakikiwa na mamlaka husika;
- (v) Kuhakikisha kwamba vyeti vyote vya kuzaliwa/vifo vimethibitishwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhadini (RITA) au wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) au Afisa aliyeteuliwa ili kuthibitisha uhalali huo;
- (vi) Kuhakikisha wanafunzi waliozaliwa nje ya nchi au wanafunzi ambao wazazi wao wamefariki dunia wakiwa nje ya nchi wanaambatanisha barua ya uthibitisho kutoka RITA;
- (vii) Waombaji wajaze fomu zao na kuzisaini kabla ya kuziwasilisha;
- (viii) Hakikisha taarifa za benki zimejazwa kwa usahihi kwenye fomu ya maombi ya mkopo;
- (ix) Maombi ya mikopo yanapaswa kuwa na taarifa sahihi na za kweli;
- (x) Waombaji wote wanatakiwa kutunza nakala ya fomu ya maombi ya mkopo waliyowasilisha Bodi ya Mikopo kwa matumizi mengine (kama itahitajika);
- (xi) Waombaji wote wanakumbushwa kuzingatia muda wa mwisho wa kutuma maombi.

02 Kwa Ufupi

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilianzishwa mwaka 2004 kupitia Sheria ya HESLB (SURA 178) na kuanza kazi rasmi Julai, 2005. Bodi ya Mikopo ina jukumu la kutoa mikopo au ruzuku kwa wanafunzi wahitaji waliokidhi vigezo.

Dirisha la maombi ya mikopo kwa mwala 2022/2023 litafunguliwa kuanzia tarehe 15 Julai, 2022 hadi tarehe 30 Septemba, 2022.

03 Stahiki

Sheria na kanuni za Bodi ya Mikopo zimeainisha sifa na vigezo vya jumla kwa wanafunzi wahitaji wa mikopo. Mwombaji STAHIKI na MHITAJI anaweza kuomba mkopo /ruzuku ili kugharamia sehemu au gharama zote za masomo ya elimu ya juu.

3.1 Mwombaji Mhitaji

Mbali na sifa za jumla, vigezo vya ziada vinafafanua mwanafunzi MHITAJI asizidi umri wa miaka 35 katika kipindi anachoomba mkopo, ambaye ni:-

- (i) Yatima (aliypoteza wazazi wote wawili) au aliyepoteza mzazi mmoja, awasilishe cheti cha kifo kilichothibitishwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) au Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA);
- (ii) Mwombaji mwenye ulemavu awasilishe fomu ya ulemavu (SDF -1) iliyothibitishwa na Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO), Mganga Mkuu wa Mkoa (RMO) au mtaalamu wa afya anayetambulika.

- (iii) Mwombaji mwenye mzazi aliye na ulemavu awasilishe fomu ya ulemavu ya mzazi (SDF 2) iliyohibitishwa na Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO), au Mganga Mkuu wa Mkoa (RMO) au mtaalamu wa afya anayetambulika.
- (iv) Mwombaji anayetoka kwenye familia ya kipato cha chini au kaya maskini ambapo elimu yake ya sekondari au stahabada (diploma), alifadhiliwa na taasisi inayotambulika, kikundi cha kijamii au watu binafsi, wanatakiwa kuthibitisha ufadhili huo.

Waombaji wa aina hii wanatakiwa kupakua fomu ya ufadhili (SCSF-3) kutoka katika tovuti ya HESLB (www.heslb.go.tz) ambayo itajazwa na mfadhili na iambatanishwe na nyaraka nyingine za maombi ya mkopo katika mtandao. Fomu zote za ufadhili zithibitishwe na taasisi husika.

- (v) Mwombaji anayetoka kwenye familia ya kipato cha chini au kaya maskini inayohudumiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) anatakiwa kuandika namba ya TASAF na kuambatanisha nakala ya kitambulisho cha TASAF kama uthibitisho wa uhitaji wake.

3.2 Sifa za Jumla ambazo zinatambulika kisheria

Vigezo vya jumla vinamtaka mwombaji mkopo atimize masharti yafuatayo:

- (i) Awe Mtanzania;
- (ii) Awe ameomba mkopo kupitia mfumo wa maombi ya mkopo (OLAMS);
- (iii) Awe amedahiliwa katika taasisi ya elimu ya juu yenye uthibati, kwa muda wote (full time)

- (iv) Kwa Wanafunzi wanaodahiliwa kusoma katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Open University of Tanzania), mwanafunzi mhitaji atalipiwa ada ya masomo, vitabu na viandikwa;
- (v) Asiwe na ufadhili mwingine kwa masomo yake ya elimu ya juu;
- (vi) Kwa waombaji wa shahada ya kwanza, asiwe ameajiriwa na serikali au na sekta binafsi;
- (vii) Awe ni mwanafunzi anayeendelea na masomo ambaye matokeo/taarifa za matokeo zinazoonesha ufaulu wa masomo yake ili kumwezesha kuendelea na masomo mwaka unaofuata au kwenda hatua nyingine ya masomo;
- (viii) Kwa mwanafunzi mnufaika ambaye anataka kuomba tena mkopo baada ya kusitisha masomo/chuo anatakiwa alipe angalau asilimia 25 ya fedha ya mkopo aliokuwa amekopeshwa awali kabla hajaomba mkopo mpya. Malipo ya asilimia 25 ya mkopo wa awali siyo dhamana ya kupangiwa mkopo.

3.3 Vigezo na stahiki nyingine

- (i) Mkopo utatolewa kwa kuzingatia uhitaji, programu na ufaulu;
- (ii) Waombaji wapya ambao kwa sasa wanaendelea na masomo, lazima wawe wamehitimu elimu ya kidato cha sita (ACSEE) au stashahada (diploma) ndani ya miaka mitano, kuanzia mwaka 2018 hadi 2022.
- (iii) Waombaji wote waliodahiliwa kusoma shahada mbalimbali kwa mwaka wa masomo 2022/2023 wanapaswa wawe wamehitimu kidato cha sita/stashahada au sifa nyingine linganishi katika kipindi cha miaka mitano, yaani kati ya 2018 na 2022.

04

Kwa Ufupi

Baada ya kuainisha waombaji wa mkopo na kuonesha taratibu katika kipengele 3.1 na 3.2 hapo juu, waombaji wa programu za masomo zenye vipaumbele zifuatazo watapewa mikopo kulingana na uwepo wa fedha.

4.1 Kundi la Kwanza

Kozi katika kundi la kwanza ni: -

- (i) Ualimu wa Sayansi (Fizikia, Kemia na Baiolojia), Ualimu wa Hisabati na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA);
- (ii) Sayansi za Afya: Udaktari, Upasuaji Meno, Dawa za Mifugo, Ufamasia, Uguzi, Ukunga, Shahada ya Sayansi katika Prosthetikia na Mifupa, Shahada ya Sayansi katika Mazoezi ya Viungo, Shahada ya Sayansi ya Afya na Maabara, Shahada ya Sayansi ya Maabara na Matibabu na Shahada ya Sayansi ya Teknolojia ya Mionzi;
- (iii) Programu za uhandisi: Ujenzi, Mitambo, Umeme, Uchimbaji Madini, Utengenezaji Nguo, Kemikali na Usindikaji, Kilimo, Chakula na Usindikaji, Magari, Viwanda, Usafiri Majini, Teknolojia ya Uhandisi wa Baharini, Elektroniki na Mawasiliano, Usindikaji na Huduma Baada ya Mavuno, Maji na Umwagiliaji, na Uhandisi wa Ndege;
- (iv) Jiolojia ya Petroli, Kemia ya Petroli; Mafuta na Gesi
- (v) Kompyuta, Programu za Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mitandao,
- (vi) Takwimu Bima (Actuarial and Data sciences)
- (vii) Kilimo, Misitu, Sayansi ya Wanyama na Uzalishaji.
- (viii) Shahada ya Awali ya Sanaa katika Kiswahili.

4.2 Kundi la pili

Kozi katika kundi hili ni: -

- (i) Programu za msingi za sayansi: Shahada ya Sayansi kwa ujumla katika Wanyama, Mimea, Kemia, Fizikia, Baiolojia, Baiolojia ya Viumbe Vidogo, Baiolojia ya Mifugo na Bioteknolojia, Uvuvi na Mifugo, Sayansi ya Mazingira na Uhifadhi, Matibabu, Hisabati na Takwimu, Sayansi ya Mazingira na Usimamizi, Afya na Mazingira, Bioteknolojia na Maabara, Wanyamapori na Uhifadhi, na Kompyuta; TEHAMA, Vipimo na Mizani, Mazingira na Maendeleo ya Miji.
- (ii) Programu ya Sayansi ya Ardhi: Ubunifu Majengo, Ubunifu Mandhari nje ya Majengo, Usanifu ndani ya Majengo, Uchumi Ujenzi, Mipango Miji na Vijiji, Usimamizi na Uthaminishi Ardhi, Jiospasho, Teknolojia katika Usanifu.

4.3 Kundi la Tatu

Programu katika kundi hili ni:

- (i) Masomo ya Biashara na Uongozi, Sayansi za Jamii, Uhasibu, Masoko, Fedha, Uchumi, Takwimu, Mazingira, Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Masomo ya Maendeleo, Sosholojia, Sayansi ya Siasa, Sanaa, uchoraji, sayansi ya ubunifu, Muziki, Sheria, Lugha, Fasihi, Jiografia, Saikolojia, Anthropolojia, Akiolojia na Masomo ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano.
- (ii) Programu nyingine zote ambazo hazijaorodheshwa katika kundi lolote kati ya hayo matatu, zitaangukia katika kundi la tatu.

Bodi ya Mikopo inaweza kulipia gharama za baadhi au vipengele vyote hapo chini: -

- (i) Gharama za chakula na malazi;
- (ii) Ada ya mafunzo;
- (iii) Vitabu na viandikwa;
- (iv) Mahitaji maalumu ya kitivo;
- (v) Utafiti;
- (vi) Mafunzo kwa vitendo.

5.1 Kipima/king'amua uwezo

- (i) Kipima uwezo kitatumika kuonesha uhitaji wa kifedha wa mwombaji.
- (ii) Malipo ya ada iliyolipwa shule za sekondari (CSEE, ACSEE) pamoja na/au stashahada (diploma) ni kigezo kimojawapo kinachoangaliwa kubaini uwezo wa kuchangia gharama za elimu ya juu.
- (iii) Vingine vinavyopima uwezo ni uyatima, ulemavu, ufadhili na familia maskini.
Kwa maana hiyo, uhitaji utapimwa kwa tofauti kati ya gharama za mwaka katika programu ya elimu ya juu katika taasisi husika ya elimu ya juu dhidi ya gharama iliyotumika kulipia elimu ya sekondari au stashahada (diploma) na uwezo wa mwombaji alioubainisha katika elimu ya sekondari au stashahada kama ishara ya uwezo wa mwombaji kuchangia gharama za elimu ya juu.

5.2 Mgawanyo wa fedha katika vipengele vya mikopo

Upangaji mikopo kwa waombaji waliofanikiwa kupata mikopo utagawanywa kwa kuanza na gharama za chakula na malazi, ikifuatiwa na ada ya mafunzo, kisha vitabu na viandikwa vikifuatiwa na mahitaji maalumu ya kitivo, utafiti, na mwisho mafunzo kwa vitendo, kulingana na kiasi cha fedha kilichobakia kutoka vipengele vilivyotangulia.

5.2.1 Chakula na Malazi

HESLB inatoa mikopo kwa ajili ya chakula na malazi kwa kiasi cha shilingi 8,500.00 kwa siku wakati wa mafunzo chuoni ndani ya mwaka wa masomo

5.2.2 Kiwango cha Ada ya Mafunzo

HESLB inatoa kiwango cha juu cha ada cha shilingi 3,100,000.00 kwa mwaka kulingana na gharama za vyuo vikuu vya umma na aina ya programu zinazotolewa.

Kiwango cha juu cha ada ya mafunzo kwa waombaji wote watakaofanikiwa kupata mikopo kitakuwa sawa na gharama za ada ya mafunzo zilizoidhinishwa kwa mwaka huu zinazolipwa katika taasisi za umma za elimu ya juu.

5.2.3 Gharama za vitabu na viandikwa

Kiwango cha juu cha shilingi 200,000.00 kwa mwaka kwa vitabu na viandikwa hutolewa kwa wanafunzi wenye sifa na wahitaji.

5.2.4 Mahitaji Maalum ya Kitivo

Kwa kuzingatia king'amua uwezo, Bodi inatoa hadi asilimia mia moja (100%) kwa ajili ya mahitaji maalumu ya kitivo kwa programu zenye mahitaji maalumu ya kitivo zilizoidhinishwa na TCU/NACTVET kwa kuzingatia viwango vilivyoidhinishwa kwa vyuo vya umma.

Wanafunzi wahitaji wenye ulemavu watapatiwa fedha kwa ajili ya mahitaji maalumu ya kitivo ili kukidhi mahitaji yao kwenye mafunzo kama itakavyoidhinishwa na Bodi.

5.2.5 Mafunzo kwa vitendo

Bodi inatoa kiasi cha shilingi 10,000.00 kwa siku hadi siku 56 kwa mwaka, kwa ajili ya Mafunzo kwa Vitendo. Mikopo kwa ajili ya Mafunzo kwa Vitendo haitafuata utaratibu wa kutumia kipima uwezo.

Mikopo kwa ajili ya Mafunzo kwa Vitendo itatolewa kwa programu zenye Mafunzo kwa Vitendo kama zitakavyopendekezwa na vyuo na kuidhinishwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

5.2.6 Gharama za Utafiti

HESLB inatoa hadi asilimia mia moja (100%) ya gharama za utafiti kwa baadhi ya programu kulingana na viwango vinavyotumiwa na vyuo vya umma vilivyoidhinishwa na TCU or NACTVET. Programu hizo ni:-

- Sayansi ya Afya
- Uhandisi
- Kilimo
- Sayansi ya Ardhi

- Programu nyingine zinaweza kupata mkopo kwa ajili ya utafiti kwa kiasi cha shilingi 100,000.00 katika mwaka wa mwisho wa mafunzo

5.3 Wanafunzi wanaoendelea na masomo na ambao ni wanufaika wa Mkopo

Kwa wanafunzi wote wanufaika wa mikopo wanaoendelea na masomo wataendelea kupokea mikopo kama awali kulingana na ufaulu wa mitihani yao. Ikumbukwe kuwa, wanafunzi wanufaika wanaoendelea na masomo ni pamoja na wale walioahirisha masomo lakini walipangiwa mikopo, wakasajiliwa chuoni na kulipwa sehemu ya fedha zao kabla ya kuahirisha masomo yao.

Kuanzia mwaka wa masomo wa 2022/2023, kila mwanafunzi mnufaika wa mkopo wa mwaka wa pili ANAHIMIZWA kuwasilisha namba yake ya Kitambulisho cha Taifa (NIN), namba yake ya Usajili wa Chuo na taarifa za Akaunti ya Benki kabla ya malipo kufanyika.

5.4 Utaratibu wa malipo

Gharama za chakula na malazi, vitabu na viandikwa, mahitaji maalumu ya kitivo mafunzo kwa Vitendo na gharama za tafiti zitalipwa moja kwa moja kwa mwanafunzi wakati ada ya mafunzo italipwa moja kwa moja kwenye taasisi husika ya elimu ya juu.

Ikitokea mwanafunzi hajasaini kwa wakati, mkopo utarejeshwa HESLB baada ya siku 30 kutoka tarehe ambayo mnufaika alitaarifiwa kuhusu malipo hayo. Kiasi kilichorejeshwa hakitarudishwa kwa mwanafunzi na hakitakuwa sehemu ya deni lake. Malipo yoyote yatakayofuata lazima kuwe na uthibitisho kutoka chuoni.

06 Masharti mengine

6.1 Wajibu wa wadhamini na wazazi

Wazazi na wadhamini wana wajibu wa kuthibitisha usahihi wa taarifa zao binafsi ambazo zimewasilishwa katika fomu ya maombi ya mkopo kabla ya kusaini. Wadhamini wanatakiwa kuhakikisha mikopo inarejeshwa na wanapaswa kufahamu mahali wakopaji walipo na ikitokea mnufaika hajamaliza kulipa, mdhamini atalazimika kulipa mkopo huo.

Mwombaji wa mkopo anapaswa kuambatanisha picha ya mdhamini na nakala ya kitambulisho kimojawapo kati ya hivi ambacho kimethibitishwa na hakimumu au wakili:

- i. Kitambulisho cha Taifa
- ii. Kadi ya mpiga kura
- iii. Leseni ya udereva
- iv. Pasi ya kusafiria
- v. Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi

6.2 Urejeshaji mikopo

Baada ya kuhitimu au kusitisha masomo ya elimu ya juu, mnufaika wa mkopo atatakiwa kurejesha mkopo kwa makato si chini ya asilimia kumi na tano (15%) ya mshahara wake wa kila mwezi.

Mnufaika ambaye amejiajiri anapaswa kurejesha mkopo wake kwa kiwango kisichopungua shilingi laki moja (100,000/=) kwa mwezi au asilimia 10 ya pato lake linalotozwa kodi. Mikopo yote inatozwa asilimia moja (1%) ya ada ya uendeshaji kwenye deni la msingi la mnufaika itakayotozwa mara moja.

07

Kuhama chuo au programu ndani ya chuo

Wanufaika wa mikopo wanashauriwa kutohama chuo kimoja na kwenda kwingine au programu moja kwenda nyingine isipokuwa pale tu ambapo haiepukiki.

Baada ya kupokea uthibitisho wa uhamisho wa mwanafunzi kutoka kwa mamlaka husika, uhamisho wa mkopo utafanyika. Hakuna uhamisho wa mkopo utakaofanyika zaidi ya siku mia moja ishirini (120) baada ya kutangazwa taarifa za udahili.

Uhamisho wa mkopo utafanyika kulingana na kiasi cha mkopo kilichopangwa awali.

7. Orodha ya waombaji waliopangiwa kwenye taasisi za Elimu ya Juu

HESLB itazingatia maombi ya mkopo kutoka kwa wanafunzi waliodahiliwa katika Taasisi za Elimu ya Juu na kuthibitishwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kupitia kwenye API.

08

Jinsi ya kuomba mkopo

Maombi yote ya mkopo yatafanyika kupitia Mfumo wa Maombi na Usimamizi wa Mikopo (OLAMS). Waombaji wote wa mikopo WANAKUMBUSHWA kutumia namba ileile ya Mtihani wa Kidato cha Nne iliyotumika wakati wanapoomba udahili.

Baada ya kukamilika kwa mchakato wa maombi kwenye mtandao, waombaji watapaswa kutoa nakala za fomu za maombi na mikataba ya mkopo kwenye mtandao, kugonga mihuri sehemu husika, kusaini fomu, na kuambatanisha nyaraka zinazohitajika kwenye mtandao wa OLAMS

Waombaji wanakumbushwa kutunza nakala ya fomu za maombi, viambatanisho vilivyowasilishwa na risiti ya EMS iliyotumiwa kutuma maombi yao kwa kufuatilia HESLB endapo itahitajika kabla ya kutuma maombi hayo kwa njia ya EMS kwenda kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo,
Eneo la TAZARA, S.L.P 76068,
15471 Dar es salaam, TANZANIA.

09

Ada ya maombi ya Mkopo

Waombaji wanapaswa kulipia ada ya maombi ya mkopo ya kiasi cha shilingi elfu thelathini (30,000.00) kupitia GepG kwenye namba ya kumbukumbu ya malipo wanayoipata katika mfumo na kulipia kupitia Benki za NMB, CRDB, TCB au kwa mitandao ya simu ya M-PESA, TIGO PESA, na AIRTEL MONEY. Kwa maelezo zaidi tembelea: <https://olas.heslb.go.tz>

10

Mwisho wa kupokea maombi

Dirisha la maombi ya Mkopo kwa mwaka 2022/2023 litafunguliwa kuanzia tarehe 15 Julai, 2022 hadi tarehe 30 Septemba, 2022. Mwongozo huu utapatikana katika tovuti (www.heslb.go.tz) kuanzia Julai 15, 2022 ili kuwawezesha waombaji kusoma kabla ya kuanza kuomba.

10.0 KUKATA RUFAA

Orodha ya waombaji watakaopangiwa mikopo itatangazwa kwenye tovuti ya HESLB: www.heslb.go.tz na kwenye akaunti za kudumu za waombaji mikopo za SIPA.

11

Orodha ya waombaji watakaopangiwa mikopo

Waombaji ambao hawataridhika na viwango vya mikopo watakayopangiwa wanaweza kukata rufaa kwa kujaza fomu za rufaa kwenye mtandao (OLAMS). Maelezo zaidi yatatolewa baadaye. Rufaa zitakazoshinda zitategemea uwepo wa fedha.

12

Maulizo na malalamiko

Waombaji au wanufaika wa mikopo wenye maswali au malalamiko watapaswa kufuata taratibu zilizotolewa kwenye dirisha la maombi ya mkopo.

Imetolewa na:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
JULAI, 2022

Uombaji Mikopo
2022/2023

TAREHE MUHIMU
Julai 15 - 18

Waombaji kusoma Mwongozo
katika www.heslb.go.tz

Julai 15 - Septemba 30

Mfumo wa kuomba mkopo
www.olas.heslb.go.tz
kuwa wazi Septemba 30, 2022
Mfumo kufungwa